SEPTEMBA MMXXV - TOLEO LA XLVI

# NGURUMO
*ya Mwandishi*







## WAPE UPENDO

**HABARI KUU:**
- Watoto wa Miono wapokea Vitabu
- KITABU MAISHA kuleta mapinduzi ya usomaji wa vitabu nchini

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
WAPE UPENDO

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
ABYAS MZIGUA

**NEW IN TOWN: Uk 04**
THE GARDEN GIRL na CARING IS SHARING

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
CHUNGU TAMU—1

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
DHIBITI UWEZO WAKO WA KUTAWALA

**MAKALA: Uk 08 - 09**
JINSI AKILI UNDE (AI) INAVYOWEZA KUMSAIDIA MWANAFASIHI

**KUELEKEA 14/10/2025: Uk 10**
MIAKA 26 BILA MWALIMU NYERERE

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
SELINA BANZI

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '8'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '8'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
Alibaba na Wezi 40 '23'

**HABARI MOTO: Uk 17**
WATOTO MIONO WAPOKEA VITABU

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
KITABU CHA TAO TE CHING

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
THE RICHEST MAN IN BABYLON

**MATANGAZO: Uk 20**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
TUNAKUKUMBUKA BABA

**HABARI PICHA: Uk 22**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
MIAKA 26 BILA MWALIMU NYERERE—2

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI (4): MARAFIKI WA MTOTO

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '10'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '05'

## TAHARIRI:
# WAPE UPENDO

Amani iwe kwenu,

Kwa kweli tuna kila sababu ya kumpa Mwenyezi Mungu Shukrani, kwa kuwa ametufikisha tena kwenye toleo letu la Sep temba linalotukumbusha 'WAPE UPENDO'

Kiukweli, kama sote tunapenda kumfikia aliyetuumba, hatuna budi kuwa na upendo kwa jirani. Inawezekana hatumjui jirani yetu kwa namna moja au nyingine. Lakini twapaswa kile t unachopata kugawana na Yule aliye kando yangu.

Katika toleo hili tunawapongeza sana taasisi ya Mar'z pamoja na Anna Mbise Pan African Mobile library kwa kuonesha up endo kwa watoto wa Miono. Kwa mwingine imekuwa kama haina maana sana lakini kwa uoande wetu tumeona toka ndani upendo ulifikishwa kwa watoto hawa. Kwa namna moja au nyingine ndiyo twasema kuwa ni kurudisha kwa jamii.

Kwakweli tunakupongezeni sana. Na hii iwe chachu kwa wadau wengine kujitolea kwa namna hiyo. Tusifikiri kuwa walemavu au watoto hawapendi kusoma. Tunakosea sana! Hili ni tabaka la watu wanaopenda sana kusoma. Kusoma kitabu hakubagui ulemavu au uzima wa mtu isiopokuwa tu ajue kusoma.

Wape upendo, usiwadharau.
Wape upendo, wajali.
Wape upendo, utashuhudia maajabu.
Wape upendo wakuoneshe upendo.

Endele kuburudika...

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

# MWANDISHI WETU:

## Abyasi Mzigua (Marudio)

**Katika toleo hili la 47, tumeona tumrudie mwandishi matata kabisa Abyas Mzigua. Mwandishi mwenye maneno mengi mtandaoni anayezikonga nyoyo za wasomaji kwa lugha yake laini na tamu.**

**Hii ilichapwa katika toleo la 16. karibu tuendelee...**



Naam!
Mimi ni ABYAS MZIGUA. Wasomaji wangu wote wananifahamu hivyo. Pia baadhi ya wadau wa fasihi nchini wanaamini hilo ndilo jina langu halisi. Kitu ambacho sio kweli.

Jina langu ni ABDALLAH YAHYA SUFIAN, nikachukua herufi mbili kwenye jina la mwanzo na kupata AB, mbili kwenye jina la pili nikapata YA, na S ya mwishoni akatokea ABYAS.
Kisha MZIGUA likafuatia kutokana na kabila.

Mimi nilianza kuandika miaka saba iliyopita. Na hatua yangu ya awali ilikuwa ni *Facebook*. Niliandika mno huko, bila ya kubeba malengo yoyote. Niliandika tu ili watu wapende...
Baadaye, nikaona kuwa kuna kitu naweza kufanya. Kikubwa zaidi. Nikaanza kusaka maarifa ya uandishi na kujifunza. Ni hapo ndipo ubora ulipokuja na kuanza kutambulika kwa ukubwa.

Mpaka sasa nina vitabu 16 kwenye vichwa vya hadhira. Lakini ndani ya hazina yangu nimeshaandika zaidi ya vitabu thelathini. Na naendelea kuandika siku baada ya siku.
Kiukweli uandishi umenipa kitu kikubwa sana maishani.
Changamoto za uandishi ni nyingi sana. Nyingi mno. Kutoka kwa wasomaji, kutoka kwenye fasihi yenyewe na kutoka kwa waandishi wengine.
Ni nyingi sana, hata nikiziorodhesha zinaweza zisienee, lakini, jambo bora zaidi nililojifunza na naweza kuwashauri waandishi wachanga kupitia changamoto, wazitazame kama fursa za kuwainua na kuwapigisha hatua.
Binafsi huwa sifichi. Hakuna mwandishi ninayemkubali kama GEORGE IRON MOSENYA. Huyu jamaa ni mtu kamili kabisa katika tasnia hii.

Sijali ikiwa ni wa zamani ama wa sasa, lakini, naamini ninapotakiwa kulitaja jina la mwandishi mwingine kwa uzuri mbele ya umati, basi jina lake linapaswa kutangulia katika mstari wa mbele.

Kazi za waandishi wa zamani zilijaa uhuru sana katika ubunifu. Mikasa yao ilikuwa iko wazi kwa sababu visa vingi vilikuwa havijaandikwa bado. Tofauti na sasa, waandishi wa miaka yetu wanasumbua mno vichwa vyao ili kupata mfululizo bora wa matukio na visa vyenye kukamata hisia za wasomaji.

Pamoja na hilo, bado waandishi wa zamani tunawatazama kama msingi muhimu ya hii nyumba tunayoendelea kujenga. Pengine, pasi na wao kushika kalamu na kuandika, labda pasingekuwa na waandishi nchini.

Mimi kwa upande wangu, mpaka sasa nina zaidi ya vitabu hamsini ndani. Vimekamilika. Vile nilivyovitoa hadharani ni vitabu kumi na sita. Mpaka sasa tunapozungumza. Na kati ya hivyo, kiukweli nachelea mno kusema kipi ni bora kuliko vyote.
Kuhusu soko, kiukweli kabisa, mimi ninayo namna yangu binafsi ya kuuza. Nikisema mauzo, soko likiwemo ndanimwe. Nashukuru, kwa upande wangu mauzo yanafanyika.

Wasomaji wananunua mno vitabu vyangu.
Ama kwa kuwa bado sijawa mwandishi mkubwa sana, huenda nikawa sijaielewa changamoto hii kwa ukubwa zaidi. Ila mpaka hapa, kiukweli kabisa, soko kwangu naona lipo kawaida.
Japo si sawa na sanaa nyingine kama muziki na filamu.
Kwa wale ambao watapenda kuzisoma kazi zangu, namna bora na nyepesi zaidi ni kuwasiliana nami kupitia namba-ri ya Whatsapp, 0688589070.

Nauza nakala tepe na nakala ngumu. Vitabu vingi vikiwa ni vya kipelele*zi*.

# NEW IN TOWN :

## THE GARDEN GIRL na SHARING IS CARING

**THE GARDEN GIRL**

Huyu ndiye Janice 'The Garden Girl', msichana mdogo aliyeandika kitabu kizuri chemye maarifa mujarab kwa jamii.
Kitabu chake kinahusu umuhimu wa kutunza mazingira, kuotesha miti, maua, mazao na mbogamboga ili kuwa na afya bora.





Kama unavyoona pichani, anazungumzia yote hayo kwa vitendo; akiotesha mboga na zikiwa zimekuwa tayari kwa kuvuna.

Kitabu chake cha **THE GARDEN GIRL** kinauzwa **Tsh 10.000** na kinapatikana kwa kupiga namba hii **0766069962.** hakikisha unakipata sasa kwa ajili ya watoto wako.

Hongera sana Janice kwa kuingia kwenye ulimwengu wa fasihi.


**SHARING IS CARING**


Benedict ni mtoto ambaye anapenda sana kuona watu wanafuraha na wanapendana kusaidiana na kushirikiana. Mara nyingi hupenda kutoa msaada kwa watoto wengine pale anapoona kuna uhitaji na hata kwa watu wazima na kama hawezi huomba msaada kwa wazazi ili apate kusaidia mtu.

Siku zote anapenda kujenga mahusiano imara na kitabu chake cha '**SHARING IS CARING: Stories of my family to yours"** kimetokana na mambo anayoyapenda na ameandika namna ambavyo ameshirikiana na watu mbalimbali ndani na nje ya familia kufanya mambo mbalimbali ya kukuza upendo na mshikamano.

Pia amezungumzia kujali mimea na wanyama kwani hata yeye anafuga sungura na kutunza bustani.

Kitabu hiki faafu kabisa kwa mtoto wako kinapatikana kwa **Tsh 15.000,** piga simu namba **0766069962**






**DIWANI YA CHUNGU TAMU**

**MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI**

**WACHAPISHAJI: TPH**

**MWAKA: 1985**

**UTANGULIZI**

Chungu Tamu ni diwani iliyoandikwa na Theobald Mvungi miaka ya 1980. Katika diwani hii mwandishi anaimulika jamii na kuichunguza kwa makini.Anakosoa na kutoa mapendekezo ili wananchi waondokane na machungu yanayowaandama na kuonja utamu ambao utawafikisha kwenye kheri.Katika diwani hii mwandishi ameonesha dhahiri jinsi Uchungu na Utamu vinayotangamana katika harakati zote za maisha ya mwanadamu.Kwa ufupi,diwani hii ni kipaza sauti kinacholia kwa sauti kali kuujulisha ulimwengu juu ya uchungu unaoiandama jamii yetu ya Tanzania .

**MAUDHUI**

**DHAMIRA KUU; UJENZI YA JAMII MPYA**

Suala la ujenzi wa jamii mpya limezishughulisha fikra za wanafasihi wengi hapa Tanzania .Jamii endelevu ni jamii mpya ambayo haina ubaguzi,matabaka,uongozi mbaya,yenye kufuata misingi ya haki na usawa.Jamii iliyojikomboa katika Nyanja zote yaani kiuchumi, kisiasa,kiutamaduni na kifikra.Wanafasihi wa Afrika wanaitaka jamii hiyo ijengwe kwa kufuata misingi ya haki na usawa kwa kila mtu. Wanafasihi wa Afrika wameonesha dhahiri kuwa jamii iliyoachwa na wakoloni ilikua zimeoza na hivyo zinahitajika juhudi kubwa ili kuondoa uozo huo.

Nchini Tanzania suala la jamii endelevu lilianza mara tu baada ya kupata uhuru na kuimarishwa zaidi wakati wa Azaimio la Arusha. Watanzania walitaka wajenge jamii yenye kufuata misingi ya haki na utu,jamii isiyokuwa na matabaka,jamii yenye viongozi waliotakasika, jamii yenye demokrasia ya kweli,jamii isiyo na unyonyaji wa aina yoyote ile,jamii ambayo hatamu za uongozi zingekuwa mikononi mwa wakulima na wafanyakazi,jamii isiyo na dhuluma ya aina yoyote,n.k.Hadi mwandishi anaandika diwani hii anaonyesha kuwa jamii bado haijafanikiwa kuifikia lengo la kujenga jamii mpya.

Mwandishi ameonesha vikwazo mbali mbali vinavyokwamisha ujenzi wa jamii mpya na endelevu hapa nchini na mbinu za kujikwamua kutoka kwenye vikwazo hivyo.Mwandishi ametoa mapendekezo ambayo anaamini kuwa endapo jamii itayafuata itafanikiwa kuijenga jamii mpya na endelevu.Mbinu hizo ndizo dhamira ndogo ndogo za diwani hii kama ifuatavyo;

**1. KUPINGA DHULUMA**

Dhuluma ni tendo lisilo la haki,tendo la uonevu,ukatili au uovu. Dhuluma hupingana na haki.Suala la dhuluma hurudisha nyuma maendeleo ya jamii na hivyo ni kikwazo kikubwa cha ujenzi wa jamii endelevu.Suala la dhuluma limemshughulisha sana mwandishi wa diwani hii,katika shairi la “Chatu na kuku” Katika ubeti wa mwisho mwandishi anasema;

Basi babu akatua,

Funda akajimezea,

Mimi tama imejishikia,

Huzuni imenisaliti,

Kwa chatu kukosa dhati,

Ndipo nikapanga hizi beti,

Ziwe kama ndiyo hati

Ukumbusho wa huyu dhulumati.

Katika shiri la “Chatu na Kuku”, mwandishi amelijenga kitaswira kuonesha jinsi wakoloni (chatu) walivyoingia Afrika na kuendeleza dhuluma.Chatu amewakilisha wakoloni na kuku anawakilisha wananchi (Waafrika) walioonyonywa na kudhulumiwa na wakoloni. Mayai ya kuku yanawakilisha mali ghafi waliyodhulumu wakoloni kutoka hapa Afrika.

**Itaendelea toleo lijalo...**

# -SAIKOLOJIA-

## DHIBITI UWEZO WAKO WA KUTAWALA



**DHIBITI UWEZO WAKO WA KUTAWALA.**
Hongera kwa kuumaliza mwezi wa tisa salama, tunapouanza mwezi wa kumi nikusihi sana uwe imara katika mambo yote, iwe furaha ama huzuni jitahidi kuwa imara. Jua kujiendesha au kujiongoza katika mambo yako yote uyaendeayo na uyatendayo. Mwezi huu wa kumi, elewa nini unapaswa kufanya katika mfumo mzima wa maisha yako katika kipindi hiki kilichobakia cha kumalizia mwaka.
Mpangilio mzima wa namna gani uishi upo ndani ya ufahamu wako wa akili, wewe ndiye ujuae kuwa unataka nini kwenye maisha yako. Ikiwa umeoa au kuolewa hapo hautoishi utakavyo wewe, mpangilio mzima wa maisha yako sasa unaingiliana na wa huyo mwenza wako. Yafaa kuelewana na kusikilizana ili kwa pamoja tuyaone maisha yenu katika umoja wenu.

Tunapouelekea mwisho wa mwaka, nikusihi katika jambo moja muhimu. Mwezi wa kumi na mbili [12] na mwezi wa kwanza, miezi hii imekua na mlolongo wa changamoto nyingi sana. Kuna kipindi cha sikukuu ndani yake, nikimaanisha Sikukuu ya CHRISTMASS lakini sambamba na sikukuu hiyo pia ni nyakati ambazo wazazi na walezi wanaingia kwenye jukumu la kusomesha watoto wao. Ni kipindi ambacho unaweza kushuhudia watu wengi sana wakikosa utulivu kisaikolojia kwa jinsi mlolongo wa jambo utakavyowaende. Ni kipindi ambacho kina uhitaji mkubwa sana. Nitumie nafasi hii kukusihi na kujisihi na mimi pia, yaani mimi na wewe tuwe makini na matumizi ya pesa zetu ili inapofika miezi hiyo tusiwaone rafiki au ndugu zetu kama hawatupendi. KILA MMOJA ANA MAJUKUMU YAKE, PANGILIA MAJUKUMU YAKO ILI USIJE KUUMIA KISAIKOLOJIA.

Katika toleo hili tuangazie namna ya kuudhibiti uwezo wako wa kutawala. Nini maana ya uwezo wa kutawala?

**UWEZO WA KUTAWALA**
Uwezo wa kutawala ni ile nguvu iliyo ndani mwako ambayo inakupa kumiliki kitu au mtu mwingine.
Ni ile nguvu ya kutawala cha kwako au ulichokabidhiwa. Mfano; mke wako, watoto wako, nyumba yako, gari lako, hivyo ni vitu ambavyo wewe ni mtawala kwavyo.

Kila binadamu anapoanza kujitambua anaanza kujua pia na kuwa na kitu chake au kuwa na uwezo wa kumiliki kitu chake.
Dhibiti uwezo wako wa kutawala. Wapo watu ambao wamepewa zawadi ya kisaikolojia ya kuwa na uwezo wa kutawala akili au ufahamu wa wengine,na kutawala mali ya mtu mwingine. Kuna watu wamepata neema ya kutawala uwezo wa wengine, mfano wao ni kama wale waliopata nafasi ya kuwa viongozi, waamuzi, washauri na mume. Ikiwa upo katika nafasi hiyo jitahidi sana katika utawala wako na mamlaka yako dhibiti ule utawala au hali ya ukuu ndani yako jitahidi sana kuidhibiti ili isikufanye ukajipa u-mungu ndani yako.

Uwezo wa kutawala unaojisikia ndani yako, jitahidi sana kuudhibiti ili usitoke nje ukakuletea madhara. Wapo watu wamebarikiwa uwezo wa kutawala kiasi kwamba anauwezo wa kutamka jambo na likatokea. Wapo watu wamebarikiwa uwezo wa kutawala mawazo yao kiasi kwamba wao kile wanachokiwaza basi kinatokea. Katika kujijua kuwa unao uwezo mkubwa, kwamba unao uwezo wa kutamka na kikatokea, au ukawa ukiwaza jambo akilini mwako, huo uwezo ndio unaotakiwa kuudhibiti ili uwe wa kuleta mafanikio kwako binafsi na kwa watu wengine

- SAIKOLOJIA -

## DHIBITI UWEZO WAKO WA KUTAWALA

wakuzungukao.

Ukijigundua kuwa una nguvu ya kufanya mambo yaweze kutokea basi dhibiti sana hiyo nguvu uliyonayo ili kufanya yanayotokea kuwa na manufaa tu. Kama uwezo ulionao ni wa kuiona hatari kabla haijatokea, utumie uwezo huo kugeuza mambo yasiyo na manufaa kuwa na manufaa. Si umejijua kuwa unao uwezo wa kuwaza na ulilowaza likatokea, basi ikiwa utawaza jambo ambalo majibu yake yakawa ni ya kuleta madhara, tumia uwezo huo huo wakati huo huo ili kugeuza ubaya kuwa wema. Dhibiti hiyo nguvu ya ndani mwako, dhibiti hiyo nguvu ya kuona na kutawala ili isilete madhara au ubaya kwenye jamii ikuzungukayo. Jitahidi pia kuficha huo uwezo wako ili wengine wasijue. Maana kiuhalisia ni kuwa hiyo ni zawadi uliyopewa.

Nikutakie maisha mema yenye wingi wa baraka katika miezi hii iliyobaki ili iwe salama kwako na kwa wakuzungukao. Kumbuka, nimesema kuwa hakuna mtu ameumbwa ili kuishi maisha ya mwingine, kabla haujalaumu watu kuwa hawakusaidii lolote, jiwekee mipangilio ya kukutosheleza wewe na wale wakuzungukao na ikiwezekana na ni muhimu kuweka mipango ya kusaidia wengine.

ASANTE.

MADAM NEEMA MGAO.
+255 763 013 206.
DODOMA.
TANZANIA.

## KITABU MAISHA KULETA MAPINDUZI YA USOMAJI VITABU NCHINI

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la KITABU MAISHA lenye makao yake makuu mkoani Iringa, limedhamiria kuleta mapinduzi katika uga wa usomaji vitabu nchini. Akiongea na mwandishi wa jarida hili mapema juma lililopita, mratibu wa mradi wa 'Kitabu kama chombo cha amani' unaotarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu Bi. Prisca Mbunda ameeleza mkakati huo wakuwafikia wanafunzi takribani 150 katika mikoa mitatu tofauti ya Tanzania Bara.

"Tunataja kitabu kiwe chombo cha kujenga amani katika jamii ya Watanzania," alisema. "Tutawafikia wanafunza wa sekondari walau 150 katika mwaka ili kuwajengea uwezo na kuamsha utamaduni wa kusoma. Siyo kusoma tu kama burudani bali kusoma ili kutengeneza ujumbe wa amani kwa jamii ya Tanzania kupitia vitabu hivyo" alieleza zaidi.

Mradi huu ulio chini ya Shirika lisilo la kiserikali la Kitabu Maisha ni mradi wa kujitolea utakaoendeshwa na vijana, waalimu wa fasihi na waandishi wa vitabu. Aidha ameitaja mikoa lengwa kuwa ni Iringa, Songea na Morogoro.

Tulipohoji kwanini wameamua kufanya 'kitabu kama chombo cha amani' alieleza kuwa kutokana na hali ya taifa letu kwa sasa jamii imepoteza amani na kubaki na utulivu tu. Zliongeza kufafanua kuwa amani haiwezi kupatikana kama haki hakuna na ukosefu wa haki huleta migogoro kati ya watu na watu, watu na serikali nk. Hivyo mradi huu utawapa vijna uwezo wa kugundua migogoro inayotokana na ukosefu wa haki na kupata tamko moja ambalo kwalo litasambazwa nchi nzima kupitia vyombo vya habari mwisho wa mradi huu.

Zaidi Bi. Prisca alieleza kuwa vitabu vitavyotumika ni vya fasihi vilivyoandikwa na waandishi wa ndani wakielekezea ukosefu wa haki za kijamii, migogoro na upotevu wa amani katika mtindo ya riwaya au tamthiliya.

# JINSI AKILI UNDE (AI) INAVYOWEZA KUMSAIDIA MWANAFASIHI

**Na Agness Mahende**

Katika ulimwengu wa sasa wa maendeleo ya teknolojia, akili bandia (AI) imekuwa chombo muhimu kinachobadilisha taswira ya ubunifu na uandishi. Kwa mwandishi wa kazi za fasihi – iwe ni riwaya, tamthilia, mashairi au hadithi fupi – AI inatoa fursa mpya za kuandika kwa ufanisi, kwa ubunifu, na kwa kina zaidi. Hapa chini kuna njia kuu ambazo AI inaweza kumsaidia mwandishi wa fasihi katika kazi yake ya kila siku:

## 1. Utafiti wa Kina na Haraka

Uandishi wa kazi za fasihi mara nyingi huhitaji taarifa nyingi za kihistoria, kijamii, kisiasa au kimaadili. Badala ya kutumia muda mrefu kusoma makala na vitabu vingi, AI inaweza kusaidia kukusanya na kufupisha taarifa muhimu kwa haraka. Kwa mfano, mwandishi anaweza kuuliza AI kuhusu historia ya mzozo fulani, maisha ya jamii fulani, au maelezo ya mazingira ya kijiografia ili kupata msingi wa ukweli katika kazi yake.

## 1. Utafiti wa Kina na Haraka

Uandishi wa kazi za fasihi mara nyingi huhitaji taarifa nyingi za kihistoria, kijamii, kisiasa au kimaadili. Badala ya kutumia muda mrefu kusoma makala na vitabu vingi, AI inaweza kusaidia kukusanya na kufupisha taarifa muhimu kwa haraka. Kwa mfano, mwandishi anaweza kuuliza AI kuhusu historia ya mzozo fulani, maisha ya jamii fulani, au maelezo ya mazingira ya kijiografia ili kupata msingi wa ukweli katika kazi yake.

## 3. Uboreshaji wa Lugha na Mtindo wa Uandishi

AI inaweza kuchambua maandiko na kusaidia kuboresha sarufi, tahajia, mpangilio wa sentensi, au hata mtindo wa fasihi unaotumika. Hii humsaidia mwandishi kuhakikisha kazi yake ina kiwango cha juu cha ufasaha na inavutia kisanaa. Pia, kwa kutumia zana za AI, mwandishi anaweza kujaribu mitindo tofauti – kama ya kisasa, kishairi, au simulizi za jadi – kabla ya kuchagua njia bora zaidi ya kuelezea ujumbe wake.

## 4. Tafsiri na Upanuzi wa Wigo wa Wasomaji

Kwa kutumia AI, kazi za fasihi zinaweza kutafsiriwa kwa urahisi katika lugha mbalimbali, hivyo kumfanya mwandishi kufikia wasomaji wa kimataifa. Tafsiri hizi zinaweza kuanza kama za awali, kisha mwandishi akazipitia ili kuhakikisha



ladha ya fasihi haipotei. Hii ni faida kubwa kwa waandishi wa Kiswahili wanaotaka hadithi zao zisikike duniani kote.

**5. Uchambuzi wa Wahusika na Mandhari**

AI inaweza kusaidia katika kuchambua kwa undani uhusiano wa wahusika, maadili yao, au nguvu ya migogoro katika hadithi. Kwa mfano, kwa kuingiza muhtasari wa hadithi, AI inaweza kutoa mrejesho kama: *"Mgogoro kati ya mhusika mkuu na jamii unahitaji kuimarishwa zaidi,"* au *"Mandhari ya kijiji inaweza kutumika zaidi kuonyesha ubaguzi wa kijinsia."* Hii inamsaidia mwandishi kuboresha uhalisia wa kazi yake.

**6. Uundaji wa Vifaa vya Kujifunzia Fasihi**

AI inaweza pia kumsaidia mwandishi au mwalimu wa fasihi kuunda maswali ya uelewa, muhtasari wa kazi, au maelezo ya wahusika kwa wanafunzi. Hii hufanya kazi za fasihi kuwa nyenzo za kujifunzia, si hadithi tu za kusomwa, bali pia za kuchambuliwa kielimu.

**7. Uchapishaji na Uuzaji wa Kazi za Fasihi**

Baada ya kumaliza kazi, AI inaweza kusaidia katika kubuni jalada la kitabu, kuandika maelezo mafupi ya kuvutia kwa ajili ya soko (book blurb), au hata kutengeneza mikakati ya mtandaoni ya kuitangaza kupitia mitandao ya kijamii. Kwa njia hii, mwandishi anaweza kuwafikia wasomaji wengi zaidi bila gharama kubwa.

**8. Kuhifadhi na Kulinda Kazi za Fasihi**

AI ina uwezo wa kuhifadhi maandiko kwa usalama katika mifumo ya kidigitali yenye ulinzi wa hali ya juu. Pia, baadhi ya mifumo ya AI inaweza kusaidia kutambua wizi wa maandishi (plagiarism) kwa kulinganisha kazi mpya na maandiko yaliyopo, hivyo kumlinda mwandishi dhidi ya wizi wa fikra.

**HITIMISHO**

Akili bandia haikusudiwi kuchukua nafasi ya ubunifu wa kibinadamu, bali kusaidia kuupanua. Mwandishi mwenye maarifa na maadili ya fasihi anaweza kutumia AI kama kalamu ya kisasa – chombo cha kuongeza kasi, ubora, na upeo wa kazi yake. Uandishi utabaki kuwa sanaa ya moyo, lakini sasa unaungwa mkono na nguvu ya teknolojia.



**Je; unataka kuhaririwa, kuandikiwa (ghost writing), kuhakikiwa au kuchapiwa hadithi au kitabu chako?**

**Wasiliana nasi kwa**
**Whatsapp: 0766974865**
**Call: 0672160016**

# MIAKA 26 BILA MWL. NYERERE 'BABA WA TAIFA'



## WASIFU: MH. JULIUS KAMBARAGE NYERERE

**Waziri Mkuu Mstaafu**

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Serikali ya Tanganyika Huru kuanzia tarehe 9 Desemba, 1961 hadi tarehe 22 Januari, 1962 alipojiuzulu na kumwachia wadhifa huo Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa ili yeye aende kuimarisha TANU mikoani.

**Maisha Yake**

Julius Kambarage Nyerere alizaliwa tarehe 13 Aprili, 1922 katika Kijiji cha Butiama, Wilaya ya Musoma, Mkoa wa Mara, Tanzania. Alikuwa mmoja wa watoto 26 wa Chifu wa kabila la Wazanaki, Mzee Nyerere Burito. Alipokuwa mtoto, Nyerere alichunga mifugo ya baba yake; alipofikisha umri wa miaka 12 alianza Shule akitembea kilomita 30 hadi Musoma. Baada ya kumaliza Shule ya Msingi aliendelea kusoma Shule ya Wamisionari Wakatoliki huko Tabora.

Alipofikisha miaka 20, alibatizwa akawa Mkatoliki hadi mwisho wa maisha yake. Mapadre walibaini kipaji alichonacho wakamsaidia kusomea ualimu katika Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala, Uganda kuanzia 1943 hadi 1945. Akiwa Makerere alianzisha Tawi la Umoja wa Wanafunzi Watanganyika na pia akajihusisha na Tawi la Tanganyika African Association (TAA). Baada ya kumaliza masomo ya ualimu alirudi Tabora akawa Mwalimu katika Shule ya Sekondari ya St. Mary´s. Mwaka 1949 alipata nafasi ya kwenda kusoma kwenye Chuo Kikuu cha Edinburgh huko Uingereza akasomea Shahada ya Uzamili ya Historia na Uchumi. Alihitimu mwaka 1952. Alikuwa Mtanzania wa kwanza kusoma katika Chuo Kikuu cha Uingereza na Mtanzania wa pili kupata shahada ya elimu ya juu nje ya Tanzania.

**Ajira:** Aliporejea Tanganyika kutoka masomoni, Nyerere alifundisha Historia, Kingereza na Kiswahili katika Shule ya Sekondari ya St. Francis (Dar es Salaam) ambayo kwa sasa inajulikana kama Shule ya Sekondari Pugu. Mwaka 1953 alichaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Tanganyika African Association (TAA), Chama ambacho alikisaidia kukijenga alipokuwa mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Makerere. Mwaka 1954 alikibadilisha Chama cha TAA kuwa Chama cha Tanganyika African National Union (TANU) ambacho kilikuwa cha kisiasa zaidi kuliko cha TAA.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, Chama cha TANU tayari kilikuwa chama cha siasa kinachoongoza Tanganyika. Uwezo wa Mwalimu Nyerere uliwashtua viongozi wa kikoloni na kumlazimisha achague kufanya kazi ya siasa au abaki na kazi ya ualimu. Nyerere alisikika akisema kuwa alikuwa mwalimu kwa kuchagua na mwanasiasa kwa bahati mbaya.

- Alikuwa Muasisi wa Chama cha TANU na CCM.
- Alikuwa Muasisi wa OAU na South South Cooperation.

*Inaendelea ukurasa wa 23*

# SAKO KWA BAKO:

## SELINA BANZI: Mbobezi wa maswala ya malikale, vitabu ni burudani yake

Leo tumemleta tena kwenu mdau wa vitabu. Ingawaje kazi yake inamnyima muda lakini bado hajauweka kando urafiki wake na vitabu. Nani huyu?

Kwa kuanza, jitambulishe na utueleze kuhusu wewe kwa kifupi… yale majibu yako marefu marefu siyataki, safu hii ni fupi!

Jina langu ni Selina Banzi. Ni mkufunzi msaidizi katika chuo kikuu Cha Dodoma (UDOM). Mimi ni mpenzi wa vitabu vya riwaya hasa za kijasusi/kipelelezi. Nilianza kusoma vitabu hivi nikiwa darasa la tatu. Nakumbuka riwaya niliyoanza nayo inaitwa KIU YA HAKI.

Tangu hapo nimekuwa mfuatiliaji wa riwaya za waandishi wengi kama Richard Mwambe, Japhet Nyang'oro, Patrick C.K., Bahati Mwamba, Abyas Mzigua na wengine wengi.

Asante .... nikuulize swali, tunaposema Shubaka la Vitabu we unaelewa ni kitu Gani?

Ni kifaa/eneo ambalo mtu anatumia kuhifadhia vitabu au nyaraka zingine ni shelf hili.

Ok! Wewe unalo Shubaka la Vitabu?

Ndiyo, ninalo nyumbani… Ofisini ndio Sina ila niko kwa *process* kulipata

Hongera sana! Sasa Tuambie Shubaka lako wewe limebeba vitabu Gani? Yaani maudhui Gani?

Shubaka langu limebeba maudhui ya dini, ujasusi na upelelezi, *diaries* zenye kumbukumbu binafsi, baadhi ya *assignments* na daftari nilizokuwa natumia shuleni

Waoh safi sana... Kwa hiyo mwenyewe unaturingishia Shubaka lako! Sawa. Vitabu unavyosoma vinakusaidiaje kwa kazi uayoifanya?

Kama mwalimu vimenisaidia kujua *psychology* ya wanafunzi na watu mbalimbali, pia vitabu hivi vinakuza sana *reasoning, thinking* na *argumentation* ukiwa msomaji utaona tu mabadiliko ndani Yako.



SELINA BANZI

Vizuri mwalimu... Kweli ukiwa mwalimu lazima usome sana. Hata Mimi ninaamini kuwa mwalimu anajua Kila kitu. Tuambie harakaharaka, una vitabu vingapi?

Mh! Ngoja nikahesabu…

Eh! Kuhesabu tena! Ndo maana ninekwanbia 'haraka haraka' yaani fikiria tu utuambie

Nadhani 80 hiviii

Sasa, kuna desturi ya wasomaji na wapenzi wa vitabu kuuambia uma idadi ya vitabu wanavyosoma kwa mwaka. Je wewe kwa mwaka 2022 umeisoma vitabu vingapi?

Mwaka Jana nimesoma vitabu visivyopungua 20

Hongera sana! La mwisho, unawaambia nini wanaokusoma hapa kuhusu usomaji wa vitabu?

Usomaji wa vitabu ni mzuri sana, kwanza unakuongezea misamiati na ujuzi wa lugha yetu adhimu ya Kiswahili, pili nikupe siri, Mimi ni mmoja wa wasoma masomo kanisani... kutokana na uzoefu wa kusoma vitabu mbalimbali sijawahi tetereka, natamka maneno vizuri bila shida. Alafu Hawa waandishi wanaandika mambo ambayo baadhi yanatokea katika jamii zetu, Kuna *situation* tunapitia vipindi tofauti tofauti Sasa vitabu hivi vinaweza kutusaidia kuhusianisha na maisha yetu ya kila siku. Hivi vitabu vinatupa maarifa mengi sana.

Asante sana. Ngurumo ya Mwandishi tunakutakia usomaji mwema wa vitabu. Ni matumaini yetu kuwa wengi wamejifunza kupitia andiko lako.

# MSALITI - 08

Na. Richard Mwambe



**Ilipoishia…**

***"Hello… naongea na nani?"* sauti nzito ikapenya katika masikio ya Amata.**

**"Spark…" akajibu.**

***"Unaasemaje?"***

**"Ninahitaji kukuona nina ujumbe wako kutoka Namba Moja!" Amata akasema.**

***"Pita ndani!"* ile sauti ikamjibu. Amata akakata simu na kumtazama yule mwanadada.**

**"Nipeleke!" akamwambia. Yule mwanadada uoga ukiwa dhahiri shahiri usoni pake alimwongoza Amata kwenye ofisi ya mkuu wake ambayo asubuhi ya siku hiyo tu alipewa amri ya kutoruhusu mgeni yeyote kufika.**

**Endelea...**

Juu ya kochi kubwa la vono, lililotengenezwa na vijana wa SUMA-JKT kwa malighafi ya sponji laini, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, CDF Mlolele alikuwa kaketi, tena kajaa tele. Uso wake ulikosa utulivu kwa namna fulani lakini alijikaza. Ungemtazama ungesema hajachana nywele. Ijapokuwa zilikuwa fupi lakini zilikuwa mafungu mafungu kama mkutano wa nzi. Ni kwa sababu ya kuzisukumasukuma kwa mkono wake mara kwa mara. Na hii ilikuwa ni tabia yake pindi apatwapo na jambo ambalo limsumbua kichwa. Amata akaingia na kusimama mbele ya meza kubwa ambayo pembeni yake ndipo alipoketi mzee huyo.

"Keti!" Amata akaambiwa.

Amata akaketi kwa utulivu kabisa kwa mtindo wa kutazamana. Haraka haraka aligundua jinsi gani mkuu huyo yupo kwenye lindi la mawazo. Macho yake yalikuwa mekundu sana; kama si kwa kulia basi kwa kufikichwa mara kwa mara,

"Nipe ujumbe wangu…" CDF akamwambia Amata.

"Ujumbe gani? Mimi nimekuja tu kwako mzee tuzungumze jambo moja zito kidogo…" Amata akamwambia CDF Mlolele. Kutoka usoni pa huyo Mkuu wa Jeshi, Amata aliona mabadiliko ya mshangao wa wazi, kisha akavunja ukimya kwa kuuliza, "Au pengine ulitegemea ujumbe fulani…?" akataka kujua.

"Ndiyo! Kukaa kwangu hapa nilikuwa namsubiri mjumbe kutoka Ikulu, nilishaambiwa kuwa kuna ujumbe wangu. Sasa wewe uliposema umetoka kwa Namba Moja nikajua ni wewe," Mlolele aliongea taratibu sana. Kiujumla alikuwa mtu mtulivu, makini na mwenye ukarimu kinyume kabisa na tunavyowatafsiri watu wa kada hii. Aliubeba uanajeshi katika ubinadamu wake.

"Hapana, mimi sijatumwa na Namba Moja…"

"Sasa kwanini umesema unatoka kwa Namba moja? Wewe ni nani kabla sijakurundika ndani?" Mlolele akaongea kwa ukali. Ni wazi hakupendezwa na ugeni huo maana si alioutarajia. Lakini, badala ya kuuona uoga na hofu kwa kiumbe aliye mbele yake, aliona tabasamu lililochanua kama ua la yugiyugi likiikabili hasira yake.

"Najua una uchungu mkubwa mkuu… nimekuja kukufariji," Amata akamwambia.

"Kunifariji kwa lipi?"

"Najua kuwa umeondokewa na wapiganaji wako kumi na sita kwa mpigo, kama tusipokufariji, hakika twaweza kukukosa. Pole kamanda, naelewa kuwa gharama ya kumuunda mwanajeshi mmoja ni kubwa sana na ndiyo maana nchi nzima imeingia simanzi. Si wewe tu, hata sisi walipa kodi tumeumia sana maana ni kodi zetu ambazo zinafanya yote hayo," Amata akaongea huku tabasamu lile likisindikiza ujumbe wake.

"Wewe ni nani?" Mlolele akauliza tena.

"Mimi ni kijana wa Inspekta Simbeye…" Amata akajitambulisha.

Jenerali Wilfred Mlolele akatulia kwa jozi la sekunde. Alimjua fika huyo *'nyoka'* aliyejificha kwenye shimo la u-inspekta wa polisi. Akamtazama Amata pasi na kummaliza.

"Aaaaannnnhhhhmmm!" Jenerali Mlolele akapiga mwayo mrefu na kunyoosha mikono yake huku na kuko. Mlio wa mifupa kujiweka sawa ulisikika kwenye viungo vya mikono yake na alipojinyoosha mgongo, nao ukafanya vivyohivyo. Amata akatikisa kichwa mawazoni huku bado machoye yakiwa yamekaza kwa mtu huyo.

"Nikusaidie nini?" Mlolele akarudia swali lilelile. Mara hii alikuwa mpya kabisa.

"Samahani, nataka kukurudisha nyuma kidogo… ofisi inapenda kujua kama ni kweli Jeshi limepokea miili yote kumi na sita na kuitambua," Amata akasema.

"Siku ya jana kwenye hafla ya kuaga miili ulikuwepo?" Mlolele akauliza.

"Sikuwepo!" Amata akajibu.

"Tuliaga miili kumi na sita,

# MSALITI - 08

kumi na nne kati ya hiyo miili haikuwa tabu kuitambua ila miwili iliungua vibaya sana lakini ndugu walichukua na kwenda kuzika hivo hivo…" Mlolele akaeleza.

"Si kwamba mliwashinikiza kuzika?"

"Hapana, wenyewe waliridhia kuzika pasi na kujali huu wa nani na huu wa nani…" Mlolele alieleza. Kamanda Amata akatulia kama anayefikiri jambo fulani. "Au we unaonaje?" akagutushwa kwa swali la Jenerali.

"Aaaanh nilitumwa kuuliza hilo. Lakini, je taarifa ya vifo hivyo kutoka huko Kongo inasemaje?" Amata akahoji.

"Taarifa gani zaidi ya kuwa wamekufa kwa mlipuko wa RPG zisizopungua tatu…" Mlolele akaeleza.

"Na kuna hatua mmeshachukua?"

"Ndiyo… na hapa umenikuta nasubiri kibali kutoka kwa Rais ili tuingie hatua ya pili," Mlolele akajibu.

"Asante bwana, labda naweza kukutembelea tena siku za usoni," Amata akasema huku tayari akiwa wima. Yalikuwa ni maswali machache tu ambayo kwake kuna kitu alipata na kukihifadhi moyoni mwake. Hakupenda kukiweka wazi hadi ahakikishe. Wawili hao wakaagana na Amata akashika njia yake na kuondoka.

➭ ▌▌▌

KATIKATI ya msitu mnene uliozunguka Mji mdogo wa Kanzene, kulikuwapo nyumba moja ndogo kando kando ya makazi duni ya eneo hilo. Mvua kubwa ilikuwa ikinyesha huku vimulimuli vya radi zenye nguvu na ngurumo za kutisha vilikuwa vikipasua anga. Ndani ya nyumba hii ndogo alikuwamo mtu mmoja tu, mwanaume, mfupi mwenye macho makubwa ya duara. Pembeni ya mwanaume huyo, juu ya meza ndogo palikuwa na upanga mmoja mkali na makali yake yalidhihirishwa na upya ulionao.

Kutoka nje ya nyumba ile, zilisikika hatua za mtu anayepita kwenye matope na kuukaribia ule mlango. Jinsi ya ubishwaji wa hodi, yule mwanaume aliyekuwa ndani alimjua mgeni huyo. Akamkaribisha pasi wasiwasi wowote. Yule mtu aliingia ndani. Alikuwa na koti refu la mvua na buti kubwa zilizofika karibu kabisa na magoti. Buti hizo zilijawa matope. Akazivua na kuziweka kando. Akaondoa na lile koti na kuliweka kando, kisha akatikisa kichwa chake na kuweka nywele zake sawasawa. Alikuwa mwanamke.

"Rodette!" yule mwanaume aliita kwa sauti yake kavu huku mkono wake ukielekea chini sakafuni, jirani kabisa na kiti alichokalia. Huko, akainua chupa yake ya Primus na kupiga funda moja maridhawa huku macho yake yakimganda mwanamke huyo. "Mbona umechafuka damu kwenye vazi lako?" akamuuliza mara tu baada ya kuitua ile bia sakafuni na kuiacha kama awali.

"Kazi ulionipa ni ngumu sana Kituli…" akasema huku akiketi kwenye kiti kingine.

"Lakini umefanikiwa?" akamuuliza.

"Sijamuua ila nimemuacha kwenye hali mbaya sana," akajibu. Kituli akatikisa kichwa juu chini.


"Wapi?"

"Nilipomwacha?"

"Ndiyo!"

"Kulekule msituni, hakuna mtu atakayeweza kumuona…" Rodette akajibu, kisha akajiinamia kama mtu anayewaza jambo fulani.

"Sawa umefanya jambo zuri sana, nitatuma vijana wakammalizie… pah! Pah! Pah! risasi tatu tu za kichwa," Kituli akasema huku akiwa kakunja vidole vya mkono wake …. ***Itaendelea...***




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

**Ilipoishia…**

**Niliwaza sana ndo kusema naenda tena kupitia maisha yale yale tena kwa shangazi, wewe niliamua kufumbua kinywa changu na kuanza kumuelezea jambo moja baada ya jingine kuhusu maisha yangu**

**Endelea...**

Japo sikuwa namjua kiundani zaidi ila yeye niliona anaweza kuwa Msaada kwenye maisha yangu, nilimuelezea huku nikiwa nalia sana, kwasababu nilishindwa kuyazuia machozi yangu kwa kile ambacho nilikipitia hapo mwanzo.

Alinikumbatia humo wodini hadi pale nilipoweza kujisikia sawa, alinifuta machozi yangu na kuhakikisha uso wangu unakuwa sawa, aliahidi nisijali katika hilo hivyo yeye ana uwezo wa kunisomesha.

Sikuwa naamini kile ambacho alikiongea yeye, ukweli nilimuomba kwa mara nyingine uwenda naweza kuelewa

Naye hakuwa mbishi alirudia tena kusema hivyo, nilinyoosha mikono yangu juu kwa kumshukuru japo sikuwa na uhakika kwasababu nilimuona kama mkaka mwenye mambo mengi tukiachana na yeye kuwa daktari.

Aliniambia atafanya kila kitu ili mimi niweze kuwa na furaha, hivyo alinipatia namba yake ya simu ikiwa kutatokea tatizo lolote nisisite kumpigia, hata kwa kuomba kwa mtu maana mimi sikuwa na simu kipindi hicho.

Aliniaga pale akidai muda wake kwa yeye kuwa hapa umeisha hivyo muda sio mrefu ataingia daktari mwingine kwa ajili ya kuendelea na matatizo yangu

Ila aliahidi kila siku atakuja kuniona mpaka pale nikapoweza kuwa sawa na kurudi shule. Nilimaliza siku tatu nikiwa pale hospitali ila kila siku hakusita kuja kunijulia hali.

Hivyo nilipendezewa na ukaribu wake sijui nini kilitokea huko kwa shangazi ila kwa kipindi hicho tayari *uncle* wangu alikuwa ameshazikwa.

Nilijikaza kama mwanamke japo roho yangu ilikuwa ikiniuma sana, sikuwa na namna, hiyo ilikuwa mipango ya Mungu haiwezi kuzuiliwa

Daktari aliniambia kwa sasa nipo sawa hivyo kesho naweza kuruhusiwa kurudi shule maana hata nyumbani sikutaka kwenda nilihofia Shangazi anaweza kunitimua na alivyo hanipendi ndio kabisa.

Asubuhi iliyofuata niliamka mapema siku hiyo maana ndo ilikuwa siku yangu ya kuondoka pale hospitali, hivyo niliachiwa ungalizi na mkuu wa shule kweny mikono ya *dokta* shahdu,

Asubuhi alikuja akiwa amevalia sare zake za kazi. Ilionyesha zahiri hiyo itakuwa siku yake ya kuingia kazini, aliniomba nisikate tamaa kwani yupo kwa ajili yangu na atahakikisha ananipambania mpaka pale nikapoitimiza ndoto yangu.

Basi nilichukuliwa na kurejeshwa shule, sikuweza kwenda kwa shangazi kama vile nilivyoweza kuwaelezea niliogopa naweza kupitia magumu kuliko haya ninayoyapitia sasa .

Shahdu aliniachia kiasi cha sh. Elfu hamsini kwa ajili ya matumizi yangu, Mungu mkubwa jamani amemchukua *uncle* wangu ila kaniletea tena mtu wa muhimu kwenye maisha yangu

Nilimshukuru sana, aliniomba nisijali katika hili na wala nisiwaze, kikubwa nipiganie maisha yangu kwa kusoma.

Nilishuka kwenye gari lake nikawa nampungia mkono, *matron* alikuja kunichukua na kunipeleka bwenini kwa ajili ya kupumzika siku hiyo sikuweza kuingia darasani kwa sababu akili yangu ilikuwa haijakaa vizuri

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—08

Niliombwa nipumzike mpaka pale akili yangu itakapoweza kukaa sawa ndipo nitaruhusiwa kujumuika na wenzangu darasani

Nilipumzika takribani siku mbili bila kuingia darasani ila Judithi alikuwa bega kwa bega na mimi, hakutaka kuniona nikidondosha chozi.

Asubuhi iliyofuata nilingia darasani japo sikuwa na raha kama siku zote, sikutaka kujionyesha kwa kila mtu ila rafiki yangu Judithi alilitambua hilo

Siku zilizidi kusonga mbele ila Shahdu hakusita kuja kuniona pale shule alipopata nafasi, pale alikuwa kama mfadhili wangu hata walimu pia hilo walilitambua

Alipenda sana kunitia moyo ili nisije kukataa tamaa, ilibaki miezi kazaa kufanya mtihani wa mwisho pale shule

Nilitamani sana kwenda kumtembelea shangazi yangu. Pamoja na mateso aliyoweza kunifanyia ila bado alikuwa shangazi yangu tu.

Nilitamani sana ila Judithi alinishauri niache ujinga nijiweke *busy* na masomo yangu na wala sio kumuwazia mtu asiye na faida kwangu

Roho yangu ilikuwa inaniuma sana, hivi kwanini shangazi aliamua kunifanyia mambo ya kikatili kama yale, hata nikisema niende ni sawa na bure, maana hata yule ambaye ningesema niende kumtembelea hakuwepo duniani.

Nilikuwa naumia sana ila sikuwa na namna zaidi ya kukubaliana na maisha yangu, uwenda Mungu aliniandikia hivyo kiasi kwamba hata nifanye nini maisha yangu bado yangelikuwa yale yale tu.

Nilijiweka *busy* sana na kusoma ili huku mbeleni nije kuwa na kazi zangu sikutaka tena maisha ya kulelewa. Miezi ilizidi kusonga mbele maisha yangu siku zote yalikuwa maisha ya kusaidiwa tu

Mtihani uliwadia usiku sikuwa nalala kabisa nilikuwa mtu wa kushinda nasoma na kulala nasoma. Sikutaka kumuangusha kabisa *uncle* wangu japo kashakuwa marehemu ila nashukuru alinikomboa sana. Bila yeye maisha yangu yangelikuwa yakutanga tanga siku zote

Sio yeye tu bali hata Shahdu pia amenisaidia sana. Ndani ya siku chache, nilipewa kile nilichokihitaji kutoka kwa Shahdu, Mungu amlipe sana popote alipo. Mnaweza kusema hii ni *story* ya kutunga, hapana bali hii ni *story* halisi

Ilibaki siku moja kufanya mtihani wa mwisho, nikiwa nimejikalia nje *matron* alikuja kukaa kando yangu, akiwa anaongea, “Shazma unajua wewe ni binti mwenye bahati sana katika maisha yako”.

“Kwanini matron?” Nilimuuliza na kutaka kujua anamaanisha nini kusema vile.

“Ukweli ni kwamba pamoja na matatizo unayoyapitia ila Mungu bado anakupenda sana, amemchukua mjomba wako ila bado kakupa mtu *spesho* kwa ajili yako, usichoke kumuomba kila siku na kuwa karibu sana na Mungu wako” alinambia.

Nilifurahi sana kusikia maneno matamu kama hayo, mara gafla simu ya *matron* iliita pale pale, “*Wow!* Kuna watu bado wanamaisha jamani tumetoka kumuongelea hivi punde na yeye anapiga,” alisema huku akiiangalia ile simu.

Sikutaka kumuuliza ni nani maana tayari kwa kuongea vile nilikuwa ni’shajua kama ni Shahdu. Matron aliniomba niipokee ila mimi sikuwa tayari kwa sababu aliyepigiwa ni yeye na wala sio mimi


Basi matron alipokea simu akawa anaongea na Shahdu mimi nilibaki kitumbua macho hata sikutaka kujua nini wanaongelea.

Ila nilishangaa kuona napewa simu. Pale, nilikuwa nahofia sana maana ndio ilikuwa mara yangu ya kwanza kuongea naye kwenye simu, ila matron aliniomba nisijali kwa sababu yeye ni mtu mzuri ana nia njema kwangu.

Nilichukua simu na kuiweka sikioni tulisalimiana vizuri akaniomba nijitahidi sana kufanya mitihani vizuri nisije nikamuambishia kwa sababu anapambana sana kwa ajili yangu.

Namimi sikutaka kumvunja moyo nilimuahidi nitafanya vizuri na wala asiwaze kuhusu hilo.

Tuliendelea kuongea pale,aliniuliza kama nime-mmiss ila nilishikwa na aibu nikashindwa cha kumjibu zaidi ya kukaa kimya tu, aliniita zaidi ya mara mbili, mama sema tu kama umenimiss... ***ITAENDELEA....***



Ilipoishia…

“**Marjane, umeokoa maisha yangu tena,” alisema. “Wewe ni muaminifu sana, ni msichana mjanja, na kuanzia sasa nakupa zawadi moja. Hautakuwa mfanyakazi wa ndani tena. Ningependa mwanangu Khalid akuoe na uwe mkwe wangu.”**

**Endelea...**

Kisha Alibaba akamgeukia Khalid.

“Yule mtu muovu ametuchezea akili zetu sote wawili mwanangu. Kwanza, aliweka alama kwenye mlango na dirisha ili aweze kurudi nyumbani hapa na kuja kuniua. Kisha akaja na kujifanya ni muuza mafuta, kumbe ndani ya mitungi yake kulikuwa na watu wenye mapanga makali! Kisha akaja kwako kwa kujifanya mfanyabishara wa vitambaa vya hariri mpaka mkawa marafiki wakubwa ilia pate nafasi ya kuwa karibu na mimi na kutimiza lengo lake. Huyu msichana wa ajabu Marjane, ameokoa maisha yetu mara zote hizo. Je utakuwa tayari kumuoa?”

Khalid akatabasamu.

“Nitamuoa Marjane, baba, kama akikubali,” Khalid alijibu. “Ni msichana mzuri, mjanja na muaminifu pia”

Kisha Khalid akamsogelea Marjane na kumshika mkono kisha akamuuliza. “Utakuwa tayari nikuoe?”

“Sawa,” Marjane alijibu.

Kisha Marjane akaangalia juu na kutabasamu kwa familia yake mpya. Hivyo basi, Khalid na Marjane wakafunga ndoa. Watu wengi walikuja kwenye sherehe. Wengi wao walikuwa ni majirani na rafiki zake Alibaba.

Katika sherehe hiyo, mmoja wa wageni alimwambia Alibaba, “Marjane ni masichana mzuri sana. lakini sio jambo la ajabu kweli kwa tajiri kama wewe kuamua mwanao amuoe mfanyakazi wa ndani?”

Kabla Alibaba hajajibu, mgeni mwengine akaingilia mazungumzo na kusema, “Marjane ni msichana mwerevu, mjanja, mpole na muaminifu. Hivyo Khalid hakuwa na haja ya kutafuta tajiri mwenzake, bali ni mwanamke bora, hivyo Khalid ana bahati ya kumpata Marjane.”

Alibaba alitabasamu kusikia hivyo na akachukua sahani nyingine ya halua na kuendelea kuburudika pamoja na wageni wake, hatimaye Alibaba alikuwa ni mtu mwenye furaha na amani.Familia iliishi kwa furaha kwa miezi mingi. Khalid aliendelea na kazi yake ya kuuza mazulia na wanawake watatu walibaki nyumbani kwa kazi za nyumbani. Alibaba hakuwa tena mkata kuni kwani bado kulikuwa na dhahabu zaidi nyumbani kwake zilizobaki. Lakini daima alikuwa akifikiria kuhusu wale wezi arobaini na hazina zilizopo mle pangoni. Hazina bado zipo?

Mwaka mmoja baada ya ndoa, Alibaba alikuwa amekaa kwenye kistuli nje ya nyumba yake, ilikuwa ni jioni iliyotulia na alikuwa akitazama watu wakitembea huku na huko.

“Angalia watu wote hawa wanaoishi mjini hapa,” alijisemea moyoni. “huenda kuna wezi wengine kati yao. Najua kwamba wale wezi arobaini walishakufa, lakini hakuna wengine zaidi ya wale kweli? Huenda wakawa bado wapo na wanaendelea na tabia ya kuiba mali na kuzificha katika lile pango. Dhahabu zangu humu ndani zimebaki chache, na nahitaji dhahabu nyingine zaidi.” Aliendelea kufikiria. “Nitakwenda pangoni kuangalia.”

Baadaye wakati wanapata chakula cha jioni, Alibaba akamwambia mkewe kuhusu mpango wake.

“Nitakwenda kesho asubuhi sana,” alisema. “Nitakwenda na punda wangu.”

“Lakini unaweza kuwa hatarini,” alijibu mkewe. “Huenda kuna wezi zaidi ya wale arobaini. Wakawa na mikuki na visu vikali. Watakuua wakikuona!”

“Nitakuwa salama, mpendwa,” alijibu alibaba. “Usihofu kuhusu mimi.”

“Basi nenda na mwanao Khalid,” Mkewe alimshauri.

“Khalid ana kazi nyingi sana za kuuza mazulia dukani kwake,” Alibaba alijibu. “Nitakwenda pangoni mwenyewe kama nilivyoenda mara ya kwanza.”

Asubuhi iliyofuata, Alibaba aliamka mapema sana, akachukua makapu sita na kuyafunga kwa wale punda wake watatu. Kisha akaiaga familia yake na kuelekea msituni.

Alipofika katika jiwe kubwa la lile pango, alisimama na kuangalia maeneo yaliyozungula pango lile. Aliuona mti mrefu ambao alijificha mara ya kwanza alipogundua pango lile.



Alisikiliza kwa makini sana – hakukuwa na sauti za kwato za farasi, wala sauti za wanyama wa porini….

Kutoka Dawati la Habari…

Septemba 27, Taasisi ya Marm'z Relationship Hub ikishirikiana na Anna Mbise Mobile Library pamoja na wadau wengine waliwafikia watoto waishio katika kituo cha kulea watoto cha Hope kilichopo Miono mkoani Pwani.

Katika tukio hilo walilolipa jina '*Operesheni Ibua Kipaji*' taasisi hizi kwa ushirikiano ziliwasilisha zawadi mbalimbali kwa watoto hao ikiwemo vitabu. Mbali na wao, wadau wengine walijumuika pamoja nao akiwemo mwanamuziki mwanaharakati Maembe Vitali.

Ziara hiyo imefuatia ombi lililofanywa na walezi wa kituo katika ziara ya kwanza iliyofanyika tarehe 8 Agosti. "Tumekuja hapa na vitabu zaidi ya mia tano vya Kiswahili na Kiingereza…" alieleza Mariam Mbano, Mkurugenzi wa Mar'z Relationship Hub.




Anna Mbise na Mariam Mbano katika picha ya pamoja.

# WATOTO MIONO WAPOKEA VITABU

Katika chapisho lake lililoidhihirisha furaha aliyonayo, Bi. Anna Mbise, Mkurugenzi na muasisi wa Anna Mbise Pan-African Mobile Library, ameandika, "Saidia watu wengine, nawe utajikuta ukiwa na furaha kwa kiwango kilekile ulichowapa wengine na zaidi." aidha alsisitiza kuwa watoto wenye ulemavu wana haki ya kufurahia usomaji hasa usomaji wa vitabu vya hadithi.



Mwisho anamaliza kwa swali "Je una furaha au ulishamwachia shetani akudanganye kuwa shida ulizonazo wewe unastahili tu kukunja uso?"

Muungano huo wa taasisi hizo mbili ulileta ladha ya aina yake katika suala zima hili la kijamii lililowagonganisha wadau wa pande zote mbili. Nyimbo, michezo, usomaji wa vitabu viliifanya siku hiyo kuwa kipekee zaidi.

Mapokeo ya watu mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii yalidhihirisha furaha na shukrani zao kwa jambo hilo na kuzitaka taasisi zingine kuiga mfano wa Marm'z Relationship Hub na Anna Mbise Pan Africa Mobiole Library katika kuirudishia jamii.

## HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—7

### TAO TE CHING

Katika toleo hili la 46 tunaendelea kucjambua historia ya vitabu ulimwenguni. Hapa tulipo ni sehemu ya 6 na baada ya kumalizana na kitabu cha Egyptian Book of the Dead, sasa tutakiangazia Kitabu cha Bhagavad Gita.

Tao Te Ching ni maandiko ya kifalsafa ya kale kutoka China, yakihusishwa na Laozi (pia huitwa Lao Tzu), ambaye anasadikika aliishi karne ya 6 KK. Ni maandiko ya msingi katika falsafa ya Utao (Daoism) lakini pia yameathiri Ubuddha, Uconfucius, siasa, sanaa na tamaduni kwa karne nyingi.

Jina lake lina maana hivi:

Tao (道) = Njia au Msingi wa ulimwengu

Te (德) = Fadhila, Nguvu ya ndani, au Wema unaotokana na kuishi kwa mujibu wa Tao

Ching (经) = Kitabu cha kale au Maandiko matakatifu

Kwa hiyo, Tao Te Ching inatafsirika kama "Kitabu cha Kale cha Njia na Fadhila."

Kina sura 81, zikiwa ni mashairi mafupi yenye hekima, mafumbo na mitazamo ya kifalsafa. Maudhui yake yanazungumzia:

Wu Wei (无为) = kuishi kwa kutoforce, kufanya mambo kwa upole, kwa mwafaka na asili.

Urahisi = kuepuka tamaa na mambo ya ziada, kuishi kwa unyenyekevu.

Uwiano wa viwili vinavyopingana = mfano mwanga na giza, nguvu na udhaifu, vipo pamoja na vinategemeana.

Uongozi bora = kiongozi bora ni yule anayesimamia bila kudhibiti mno, kiasi kwamba watu wanahisi wanaongoza maisha yao wenyewe.

Ni moja ya vitabu vilivyotafsiriwa zaidi duniani (baada ya Biblia).

Unataka nikupe muhtasari wa sura zote 81 kwa kifupi ili upate picha ya ujumbe wake mzima, au unataka mambo makuu tu ya msingi?

Sawa . Hebu nikupe muhtasari wa sura zote 81 za Tao Te Ching kwa lugha rahisi na fupi ili usome kama ramani ya hekima yake:

Muhtasari wa Tao Te Ching (81 chapters)

Sura 1–10: Kuhusu Tao (Njia)

Tao haiwezi kuelekezwa kwa maneno, ni fumbo la asili.

Kila kitu kina kinyume chake: nzuri/mbaya, kubwa/ndogo.

Usisukume watu kwa tamaa, waache waishi kwa urahisi.

Tao haina kikomo, ni tupu lakini hujaza yote.

Asili haichagui – jua linawaka kwa wote.

Tao ni la milele, kama chemchemi isiyokauka.

Utu wa kweli ni kuishi kwa ajili ya wengine, si ubinafsi.

Bora ni kama maji: linafaa kila kitu bila kushindana.

Kuzidi kupita kiasi kunaleta kuharibika.

Utulivu wa ndani ndio nguvu ya kweli.

# KITABU NILICHOSOMA

## THE RICHEST MAN IN BABYLON

**HAKIKA watu wanasoma vitabu na wanavitumia kama kiongozi wa maisha yao. Wengi wanafanikiwa sana. Leo Abigael Mwafulilwa anatujuza juu ya kitabu alichosoma. Na kitabu chenyewe si kingine bali ni The Richest Man In Babylon.**

Abigal anatuambia kwamba, baada ya kusoma kitabu hicho, yafuatayo ndiyo aliyojifunza…

**SHERIA TANO ZA DHAHABU**

1. Dhahabu huja kwa wingi kwa yule ambaye huweka akiba moja ya kumi ya kipato chake, na kuitumia kuwekeza kwa ajili ya wakati ujao.

2. Dhahabu hufanya kazi kwa bidii na kwa uaminifu iwapo itampata mtu anayeipatia kazi yenye faida. Hapo itaongezeka kama wanyama wa kufungwa.

3. Dhahabu hung'ang'ania kukaa kwa mtu anayeilinda na mwenye tahadhari. Mtu anayeomba ushauri kutoka kwa watu wenye ujuzi na uzoefu wa kuitunza.

4. Dhahabu haikai, na hupotea kwa mtu ambaye anawekeza kwenye biashara, au mradi ambao haujui vizuri, au miradi ambayo haishauriwi na wale wenye uzoefu na ujuzi wa kuitunza.

5. Dhahabu haikai kwa mtu anayeiwekeza kwenye miradi inayodai kutoa faida kubwa kuliko kawaida, wala kwa wale wanaodanganywa na matapeli na watu wajanja—wajanja, na wale ambao wanawekeza bila kupata ushauri kutoka kwa wale wenye uzoefu, au wale wanaowekeza kwa sababu wanapenda tu miradi ya aina hiyo.

Hii pia imeelezea baadh ya *tips* alizo kua anatoa Arkad kwa watu ili wawe matajiri kama yeye

Tukiongelea kuhusu zile tiba 7 alizosema kwa ajili ya pochi tupu

Ya kwanza ilikua ni kutunisha pochi yako kwa kuweka pato lako lote na kutumia 90% tu na kuacha 10% ndani ya pochi

Ya pili ni kupangilia matumiz akasisitza usichanganye matumizi na matamanio

Ya tatu ni kuzalisha sio utunze na kufanya matumizi tu

Ya nne alisema ni kuzilinda

Mpaka hapa nimekuja kuelewa ule msemo kuwa mwenye nacho huongezewa asienacho hunyang'anywa hata kile kidogo alichonacho

Arkad anasema ukiweza kutunza kiasi kidogo cha mali ulizonazo Mungu anakua na imani juu yako kuwa hata akikupa kikubwa utakitunza pia

Kwahiyo pochi itazidi kutuna.

Hakikisha unazilinda pesa zako

Usiwekeze sehemu uliyosikia kuna utajiri wa haraka, hii haipo. Kumbe kutajirika haraka wameikataa toka kale.

Kabla hujawekeza Hakikisha unachunguza unapowekeza mambo, ili mambo yakienda kombo mtaji wako unabaki salama.

Kama unafanya kukopesha watu, kopesha ambao una uhakika atakulipa ili asikuyumbishe

Sio mtu hana mishe yoyote wala ahangaiki anakuomba umkopeshe laki mara moja

Pia alisema unapotaka kufanya kitu chenye manufaa chukua ushauri kwa watu husika.

Unajenga, unaenda kuomba ushauri kwa muuza mikate !

Unataka kununua dhahabu unaenda kuomba ushauri kwa mtu ambae hajui ata mikoa yenye dhahabu iko wapi lazima ule za kichwa!

Pia akashauri tujenge yaani makazi yako yawe uwekezaji wenye faida *Means* nyumba ni mradi wa kudumu na utakua na faida hata kwa watoto wa watoto wako.

Tiba nyingine ilikua ni kuongeza pato lako. Pato utaongeza kwa kuongeza maarifa *that's obviously*.

Pia weka malengo madogo madogo kwanza na marahisi ambayo utaweza kuyatimiza.

Sio uweke lengo la kuwa kama MO' mwezi ujao, ni kitu kikubwa na kinachosha akili. Weka lengo jepesi mwisho utaweza kutimiza lile kubwa.

Tiba ya 7 ilikua n kulipa madeni kwa wakati na kuijali familia yako wasiwe na manung'uniko juu yako


Andika wosia mapema hata *ukikata moto* mali ulizoacha zigawanywe kwa usawa

Kingine ni kusaidia wasio jiweza



ABIGAIL MWAFULILWA

# HABARI PICHA



Mwandishi Isaac Ndolo (kushoto) aliyeandika Wimbo wa Yatima alipotembelea banda la Mkuki na Nyota kwenye maonesho ya Vitabu Jijini Nairobi.





Mwandishi Murori Kilunga (kushoto) alipotembelea banda la Mkuki na Nyota katika maonesho ya vitabu Jijini Nairobi.



Mkurugenzi wa Anna Mbise Mobile Library Bi. Anna Mbise akiwa katika pozi la kivitabuvitabu pamoja na mmoja wa watoto wa kituo cha Hope, Miono, mkoani Pwani.

Balozi Christopher Liundi akimkabidhi mmoja wa wateja wake kitabu alichokizindua siku hiyo ' MARA YANGU YA KWANZA'






TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## TWAKUKUMBUKA BABA

Miaka ishina sita, Baba tangu umeenda
Wanao bado twasita, kwani bado twakupenda
Jinalo bado twaita,
Twakukumbuka Baba!

Nchi umetuachia, utulivu na amani
Taifa metujengea, asiyejua ni nani
Bado hatujalegea, twapambania amani
Twakukumbuka Baba!

Mwana wa Kizanaki, mmajumui asilia
We' hukupenda kiki, Afrika lipigania
Vipi kizazi hiki, kazi kulialia
Twakukumbuka Baba!

Turithishe ujasiri, nchi kuipigania
Tutende kwa kufikiri, kile tunapambania
Uzalendo kukithiri, hiyo ndiyo yetu nia
Twakukumbuka Baba!

Uliacha kila kitu, kuitaka Tanzania
Ulitoa wako utu, uhuru kupigania
Na hukushika mtutu, maneno ulitumia
Twakukumbuka Baba!

Woga ulimjaa, mweupe akakimbia
Furaha ikatujaa, kuipata Tanzania
Ni wewe ndo shujaa, na wale walofatia
Twakukumbuka Baba!

Upumzike peponi, Mungu akokwandalia
Haya ya hapa nchini, tuombee kwa Jalia
Ili idumu amani, hapa kwetu Tanzania
Twakukumbuka Baba!

**Shujaa Maneno**
**Bagamoyo Pwani!**

## PENZI NI KITU GANI?

Wengine walililia
Wengine hawataki sikia
Wengine washangilia
Wengine waona ghasia
Kwani penzi ni kitu gani?

Wazee umri umeenda, penzi waling'ang'ania
Hamu yao tu ni tunda, kiuno kukimbilia
Mabinti nao watenda, pasi na kuaibia
Kwani penzi kitu gani?

Mabinti wataka wazee
Eti kisa wawatunze
Achene huo utezeze
Kutaka maisha yatereze
Kwani penzi kitu gani?

Mimama yataka vijana
Yatunza pasi hiyana
Hao ni sawa na wana
Watu wazima hamna mana
Kwani penzi kitu gani?

Acha penzi kupenzika
Maadili yajali rika
Ya nini kudhalilika
Mtu mzima chakarika
Kwani penzi kitu gani?

Rudisha upanga alani
Mtu mzima mpagani
Kwani penzi kitu gani
Hata uishie motoni?

**Jamila Mikasa**
**Iringa**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# TANGAZO


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu: 0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au wasiliana nasi Kwa Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
15,000/= tu
Jipatie Nakala Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

***Inatoka ukurasa wa 10:***

Alijiuzulu ualimu na kuzunguka nchini Tanganyika kuzungumza na watu wa kawaida na machifu ili kuleta muungano katika kupigania Uhuru. Pia alizungumza kwa niaba ya TANU katika Baraza la Udhamini na Kamati ya Nne ya Umoja wa Mataifa huko New York, Marekani. Uwezo wake wa kuunganisha watu ili wawe na umoja na mshikamano kutetea haki zao pamoja na kipaji chake cha kujenga hoja, kutetea na kuzungumza kwa ufasaha ulimwezesha kufanikisha Tanganyika kupata Uhuru bila umwagaji wa damu. Ushirikiano mzuri aliouonyesha kwa aliyekuwa Gavana wa wakati huo, Bw. Richard Turnbull ulisaidia pia kuharakisha upatikanaji wa Uhuru.

## Uongozi

Tanganyika ilipata Uhuru wake tarehe 9 Desemba, 1961 na Nyerere alichaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanganyika huru. Mwaka mmoja baadaye, Nyerere alikuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika. Nyerere alikuwa kiungo muhimu katika kuleta Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iliyounda Tanzania baada ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 ambayo yalimtoa madarakani Sultani wa Zanzibar, Jamshid bin Abdullah.

Mnamo tarehe 5 Februari, 1977 Mwalimu Nyerere aliongoza chama cha TANU katika kuungana na chama tawala cha Zanzibar cha Afro - Shiraz Party (ASP) na kuanzisha Chama kipya kilichoitwa Chama cha Mapinduzi (CCM) akiwa Mwenyekiti wake wa kwanza. Mwalimu Nyerere aliongoza Taifa kwa miaka 23 hadi mwaka 1985 alipostaafu na kumwachia nafasi Rais wa Awamu ya pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi. Yeye alibaki kuwa Mwenyekiti wa CCM hadi mwaka 1990 alipostaafu licha ya kuwa aliendelea kuwa na heshima kubwa katika nyanja za siasa ya Tanzania na duniani hadi kifo chake.

Mwalimu Nyerere alitumia muda mwingi kukaa kijijini kwake Butiama huku akilima shambani kwake. Pamoja na hayo, alianzisha Taasisi ya Mwalimu Nyerere Foundation mwaka 1996. Aidha, alikuwa mpatanishi wa vita vya wenyewe kwa wenyewe huko Burundi. Pia kati ya mwaka 1987 hadi 1990 alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kusini (South Commission).

## Mauti

Tarehe 14 Oktoba 1999, ni siku ambayo Taifa la Tanzania halitaisahau kamwe kwani Mwalimu Nyerere aliaga dunia akiwa na umri wa miaka 77 katika Hospitali ya St. Thomas iliyoko jijini London, Uingereza baada ya kuugua kansa ya damu. Mwili wa Mwalimu ulipokelewa jijini Dar es Salaam tarehe 18 Oktoba, 1999 na kupelekwa nyumbani kwake Msasani. Tarehe 20 Oktoba, 1999 mwili wa Baba wa Taifa ulipelekwa Uwanja wa Taifa ili Watanzania kwa ujumla waweze kumuaga mpendwa wao. Tarehe 21 Oktoba, 1999 ilifanyika sala ya mazishi ya Kitaifa katika uwanja huo ambayo iliongozwa na Muadhama Polycarp Kardinali Pengo. Viongozi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi walihudhuria ibada hiyo. Watu waliendelea kumuaga Baba wa Taifa Taifa usiku na mchana hadi tarehe 22 Oktoba, 1999 jioni mwili wake ulipoondolewa na kusafirishwa kwenda Musoma na hatimaye ukasafirishwa kwenda kijijini kwake Butiama kwa ajili ya mazishi. Mazishi ya Mwalimu Nyerere yalifanyika tarehe 23 Oktoba, 1999 nyumbani kwake huko Mwitongo katika kijiji cha Butiama, wilayani Musoma Vijijini, mkoani Mara.

### Vitabu alivyoandika Hayati J.K Nyerere

1. Ujamaa: The Basic of African Socialism - 1962
2. Freedom and Unity (Uhuru na Umoja) - 1966
3. Freedom and Socialism (Uhuru na Ujamaa) - 1968
4. Freedom and Development (Uhuru na Maendeleo) - 1973
5. Crusade of Liberation - 1979
6. Man and Development - 1974
7. Our Leadership and The Destiny of Tanzania - 1995

### Vitabu alivyotafsiri

1. Julius Caesar - tafsiri ya tamthiliya Shakespear
2. The Merchant of Venice (Mabepari wa Vennisi) Tafsiri ya Shakespear

Zaidi ya hivyo pia aliandika machapisho mbalimbali ikiwemo ushairi wa Vitabu vine vya Injili.

Huyu ndiye Mwalimu Nyerere, apumzike kwa amani.

## SAFARI YA MALEZI – 04

### 3.3 MARAFIKI WA MTOTO

### 3.3.1 Marafiki wa Mtandaoni au Marafiki wa Maisha Halisi?

Katika kizazi hiki cha kidigitali, wazazi wengi wamekuwa wakipambana na changamoto mpya isiyoonekana kwa macho – *marafiki wa mtandaoni*. Tofauti na enzi za zamani ambapo-marafiki wa mtoto walikuwa wanajulikana ni kina nani, leo hii hali ni ngumu zaidi. Unakuta mzazi anapiga marufuku mtoto wake asicheze na watoto wa jirani, asitoke nje, asihusiane na mtu yeyote katika maisha halisi. Lakini mzazi huyu hajui kuwa ndani ya simu au *tablet*, mtoto wake ana zaidi ya marafiki 1,000 wa mtandaoni, anaowaita *followers, friend's* au *fans*.

Na. KELVIN JOHN KYARA
0753767930

Sasa tujiulize, **nani bora, rafiki mmoja wa kweli au marafiki 1,000 wabaya?** Rafiki wa kweli humsaidia mtoto kujifunza ustahimilivu, uvumilivu, kushirikiana na heshima ya kijamii. Lakini marafiki wa mtandaoni ambao hawana thamani ya kimaadili, wanaweza kumshinikiza mtoto kufanya mambo mabaya, kumfanya ajione duni, au kumwingiza kwenye majaribu ya kimaisha. Mtoto anazuiwa kucheza na mtoto wa jirani anayeenda naye shule au nyumba ya ibada pamoja, na huku ana marafiki wengi mtandaoni, lakini hapewi mwongozo juu ya nani anayeweza kumfuata kwenye *TikTok, Instagram au Telegram*.

Hili ni kosa kubwa! Watoto wanaponyimwa nafasi ya urafiki wa maisha halisi, hukimbilia ulimwengu wa bandia, ambapo kuna uhuru wa uongo, uhuru wa majaribu na uhuru wa upotovu wa maadili.

Je, tunajua ni maudhui gani mtoto wetu anaangalia? Leo hii, kuna video na picha za watu waliovaa nguo zisizofunika mwili vizuri, kuna *memes* na vichekesho vilivyojaa matusi na dharau kwa jamii, familia na utu. Mtoto anapoyaona haya mara kwa mara, taratibu yanamjengea uhalisia mpya wa uongo, ambao unamfanya aamini kuwa maisha ya uhuru ni maisha ya starehe zisizo na kikomo. Kwa muda mrefu, watoto wengi wamepoteza nafasi ya kuwa karibu na familia zao kwa sababu ya kutawaliwa na urafiki wa mtandaoni. Hawana tena muda wa kushirikiana mezani, kuomba pamoja, au kujifunza maadili ya kimsingi. Hii ni hatari kubwa ambayo mzazi wa kisasa asipokuwa makini, ataishia kulea mtoto ambaye anaishi kwenye "*ulimwengu wa bandia*" badala ya maisha halisi yenye uhusiano wa kweli na watu wa karibu.

### 3.3.2 Mzazi wa Kisasa, Amka!

Kujua jina la rafiki mmoja wa mtoto wako aliyeko jirani ni bora kuliko kufumba macho kwa maelfu wa mitandaoni usiowajua. Mtoto anapokuwa na rafiki anayemjua vizuri, mzazi hupata nafasi ya kuelewa mwenendo wake, tabia zake na familia inayomlea. Lakini marafiki wa mtandaoni mara nyingi hawana uso, hawana historia inayoeleweka, na mara nyingine ni watu wazima wanaojificha kwa majina bandia.

Kupanga siku ya michezo au kutembeleana na marafiki wachache wa kweli ni bora zaidi kuliko mtoto kuwa mtumwa wa skrini mchana na usiku. Michezo ya nje hufundisha mshikamano, heshima, mashindano ya haki na staha. Lakini michezo ya mtandaoni mara nyingi huchochea

hasira, mashindano yasiyo na tija na hutengeneza utegemezi wa kifedha kwa kupitia ununuzi wa kifedha wa kimtandao (*in-app purchases*).


Mzazi wa kisasa unahitajika kuwa **mlinzi wa moyo, si mlinzi wa mlango tu.** Kumlinda mtoto kifikra na kiroho ni jukumu kubwa kuliko kumfungia ndani bila maelekezo. Malezi bora ni yale yanayojumuisha mawasiliano ya wazi, ushirikiano wa familia na mafunzo ya maadili yanayoonekana kwa vitendo.

**3.3.3 Suluhisho ni nini?**
Ili kumsaidia mtoto wako asiwe mteja wa marafiki wa mtandaoni wasiofaa, mzazi anapaswa kuchukua hatua makini. Zifuatazo ni njia rahisi lakini zenye nguvu:

**3.3.3.1 Zungumza na mtoto wako** – Mweleze madhara ya urafiki wa mtandaoni bila kumkaripia. Tumia lugha ya upendo na tahadhari. Fanya mazungumzo ya kawaida, chukua muda kumweleza tofauti kati ya rafiki wa kweli na rafiki wa mitandaoni.

**3.3.3.2 Weka muda rasmi wa teknolojia** – Si kila saa ni ya runinga au simu. Weka ratiba ya kusoma, kusali, kuzungumza kama familia na kucheza. Ratiba hii ikifuatiwa kwa nidhamu, mtoto atajifunza kupangilia maisha yake bila utegemezi wa teknolojia.

**3.3.3.3 Shirikiana na wazazi wengine** – Tengenezeni vikundi vya malezi; tembeleeni watoto, fanyeni shughuli za pamoja, michezo, kambi za familia na maombi ya pamoja. Watoto wanaposhirikiana katika mazingira ya kweli, hujenga urafiki wa kudumu na wenye maadili.



**3.3.3.4 Fundisha maadili kwa vitendo** – Watoto huiga zaidi matendo ya wazazi kuliko maneno yao. Unapomtaka mtoto awe mwaminifu, hakikisha nawe unaishi kwa uaminifu. Ukimtaka aache kutumia simu kupita kiasi, hakikisha nawe unadhibiti matumizi yako ya teknolojia mbele yake.

**Muhimu: Ni heri mtoto wako awe na rafiki mmoja mwenye maadili kuliko kuwa na marafiki 1,000 wa bandia wanaompotosha.** Mtoto anayejengewa mazingira ya urafiki wa kweli hufundishwa kupenda, kuheshimu na kuchagua marafiki kwa busara. Urafiki wa kweli humjenga mtoto kiakili, kihisia na kiroho. Usimwondolee mtoto marafiki, BALI mwelekeze kwenye marafiki sahihi, wenye mwelekeo bora wa kimaisha. Kwa kufanya hivyo, mzazi atakuwa si tu mlezi wa mtoto wake, bali pia mshauri na rafiki wa karibu zaidi.



# HAPPY NEW YEAR '10'—Twahir Yusuph

***Ilipoishia…***

**Hiyo ikawawasilishia taarifa nyingine isiyo nzuri kwenye vichwa vyao, wakaongeza kujihami. Hatua zao zikaujaza umakini, mboni zao zilipepesa kwa uangalifu mno, huku viganja vyao vikizishikilia vizuri bastola zao.**

---

**Endelea...**

Tayari kitendo cha kuiona damu kwenye kiwambaza cha nyumba hiyo kilishawachorea mstari mwembamba wa kuwepo amani ndani humo. Polepole walizidi kusogea, kwa mara pili macho yao yakashuhudia tukio lililowatisha kuliko damu walizozikuta kiwambazani. Ndiyo, walishaifikia sebule ya nyumba hiyo tayari, mboni zao zikakutanishwa na kiwiliwili cha mtu, kilichowekewa kichwa chake pembeni juu ya meza, kichwa chenye sura ileile aliyoiona pichani Inspekta. Nani kaua? Hata wao walibaki kwenye taharuki iliyowasisimua kwa woga. Ni aina ileile ya mauaji, ila huyu hakurekodiwa wala kutupiwa mtandaoni, aliuliwa kimyakimya. Haraka Inspekta akatoa simu yake mfukoni na kutoa taarifa kwa askari wengine ili waweze kufika eneo hilo.

Pia akapiga simu kwa IGP Edward Kituo, kuhusu walichokuja kukifanya pahala hapo na hadi walichokikuta. Alitoa maelezo yote kuhusu uchunguzi alioufanya, hakubakisha. Jina la Labi Kimati likasimama kama mshukiwa wa mauaji hayo ya daktari, na kwa aina ya kifo walichokikuta, hawakuwaza mara mbili kuwa ni yeye pia aliyewaua rafiki zake wawili. Wangemshuku nani sasa? Labi ndiye waliyepata taarifa kuwa anakuja huku kuonana na Daktari asubuhi hii, Daktari waliyemkuta hana maisha tena. Alieleweka Inspekta Kasese, IGP Edward Kituo akatoa kauli moja tu akamatwe. Aliyeua kwa upanga, kwanini roho yake itolewe kwa bisibisi? Hapana aletwe, akibisha apigwe risasi nyingi hadi kifo kimtetee, IGP Edward Kituo alitoa amri nyingine. Bila kupoteza muda, jeshi la askari polisi likafika eneo hilo, baadhi walishughulika na tukio lililomkuta Daktari ambaye bado jina lake halikufahamika. Wengine walijiweka tayari kwa ajili ya kwenda kuutekeleza mpango wa kumtia nguvuni mtuhumiwa wao. Tayari Labi Kimati alishatafasirika kuwa ndiye binadamu hatari na katili zaidi aliye nyuma ya mauaji yote ya kutisha nchini. Kwenye magari manne yaliyowasili sehemu hiyo, moja ilibaki kwa ajili ya kuubeba mwili wa daktari na kuufikisha pahala husika, matatu yakawashwa, yote yakisheheni maaskari waliobeba silaha za moto.

Inspekta Azizi Kasese akaongoza msafara huo wa kwenda kumtia nguvuni mtoto wa tajiri mkubwa nchini Takaseni. Safari ya kumfuatilia Labi Kimati ikapamba moto. Tayari walishashika njia, ving'ora vya gari zao vilivitawanya vyombo vingine vya usafiri barabarani, wakapishwa wao watangulie. Msako ulibidi ukaanze anapoishi. Wakiwa njiani kumfuata Labi Kimati, dakika chache baada ya kuliacha jengo la Daktari waliyeukuta mwili na roho yake viko tofauti tofauti, jina la IGP Edward Kituo linaibuka kwenye kioo cha simu ya Inspekta Kasese, haraka anaipokea na kuipachika sikioni. "Ghairisheni huo mpango sasa hivi." ni kauli ya kwanza iliyosikika simuni, ambayo ilimshangaza mno anayeambiwa. "Labi Kimati sio muuaji, na hana hatia." hii ya pili ndiyo iliyomshtua zaidi Inspekta. 10 Tughairishe kwenda kumkamata mharifu? Tena aliyehusika na mauaji ya mwanawe mwenyewe! Huyu ambaye amekuja huku kwa daktari na kumvesha kanzu ileile ya umauti! Kwanini hana hatia sasa! Swali na mishangao viliichimba njia kwenye akili ya Inspekta Kasese. "Kwanini mkuu" akaikiuka amri hiyo na kumtupia kiulizo kiongozi wake. "Washa Data." IGP Edward Kituo akatoa jibu kwa sauti tepe sana, tena nyepesi mno.

Haraka akatenda alichoambiwa, ukisikia washa data, basi kingine cha kufanya lazima ukifahamu, ndivyo alivyofanya askari huyo Azizi Kasese mwenye cheo cha inspekta. Alitembelea katika ukurasa wenye jina la KIFO mtandaoni, ni kwa adui waliyekuwa wakimfuata muda huo, katili waliyejipa uhakika kuwa si mwingine, ni Labi Kimati. "Simamisha Gari" alitoa amri hiyo mboni zake zikitawaliwa na taharuki Inspekta Kasese, zote mbili zikiwa zinamulika juu ya kioo cha simu yake. Sababu wao ndiyo vinara wa msafara huo, baada ya matairi ya gari yao kutoendelea kufanya mizunguko, gari nyingine zote zikafuata. Ameona nini hadi kimkodoleshe macho kiasi hicho? Yaleyale, ni muuaji tena na leo. Ndiyo, labda kipindi kifupi cha amani wali-

chopitia kilikuwa mapumziko, leo ilichapishwa video nyingine kwenye kurasa hiyo ya mtu asiyejulikana mtandaoni, tena akiwa mubashara sio rekodi. Kilichomshangaza zaidi Inspekta Kasese, ni kumuona Labi Kimati akiwa kafungwa kitini, amelowana damu chapachapa, yaani hatamaniki.

Pigo la pili la mshangao kwa kila aliyekuwa yupo mubashara mtandaoni kutazama tukio hilo, ni pale muuaji alipoamua kuuonesha uso wake kwa mara ya kwanza. Leo alionekana binadamu katili waliyekuwa wakimsaka vipindi vyote vya majira ndani ya siku. Mikunjo ya sura yake ilibeba hisabu ya umri mkubwa alionao, paji lake lilisheheni upole mno, haonekani kama anayo hatia ya anachokifanya! Mkononi alikamata shoka, mavazi yake yalitapakaa rangi nyekundu nzito, ni damu. Tembea yake ilikuwa ya kichovu mno akiwa ameshikilia kiti mkono wake mmoja, akakitua na kuketi kando ya Labi Kimati aliye hoi bin taabani. Macho yake aliyatupa mbele ya anachoangaliana nacho, ni kamera. Wakati yanatendeka yote hayo, yule mwanamke mrembo aliyeahidiwa na Labi kuwa atapitiwa siku hiyo, alizipata taarifa hizo, naye haraka akazama mtandaoni kuhakiki kama kweli yanayoendelea yanamtokea mwanaume wa ndoto zake au ni uvumi tu. Hakuamini! Ni kama moyo wake uliguswa na kitu chenye ncha kali kilichozama ndani na kuutoboa, alihisi maumivu makali mno Vivi, mboni zake zinamjua fika Labi wake. Ndiye yeye aliyekuwa akimtazama sasa akiwa hoi hajiwezi, pia amevunjishwa kinguvunguvu ile ahadi yao ya kukutana siku hiyo, Labi alikuwa mtekelezaji wa kila anachoahidi, hakuwa muongo.


Amefanya nini babu harusi wake mtarajiwa hadi atendewe hivyo? Ni siri ya katili na muuaji huyo aliyemteka Labi. Machozi yalimchirizika Vivi. Kwenye lile kundi la marafiki watatu, leo huyu wa mwisho naye yanamkuta yaleyale, lakini kwake imekuwa tofauti kubwa mno, amewekwa mubashara mtandaoni, sio rekodi. Pia kwenye ile picha inayowaonesha wapo watano, amebaki yeye tu hadi sasa, na haijui hatma yake. Kuna siri gani hapa?

* * *

Baada ya kuketi na kuitazama kamera, mara kikohozi kikamshika kabla ya kuzungumza chochote, kilipoacha alinyanyua mkono wake kwa ishara ya kuomba radhi, alipoushusha akauzamisha kwenye kizibao alichovaa, akatoa kitana. Polepole akaanza kuzichana ndevu zake nyingi ambazo hazikukaa kistaarabu. Akamaliza na kukirudisha, "Habari za saa hizi wananchi, na wazazi wa marehemu mnaonitazama, hadi wewe wa huyu mtoto aliye kitini hapa." muuaji akasalimia, ni sauti nzito, iliyokiacha kinywa chake bila haraka. Ukiacha Vivi na watu wengi waliokuwa wakilitazama tukio hilo la kushangaza, mzee Sesewa Kimati, CDF Rashidi Koboko, na IGP Edward Kituo wote walikuwa wakilishuhudia tukio hilo pia, hadi rais wa nchi profesa Omar Kifaranga hakuwa nyuma. Alilifuatilia. IGP akiwa makao makuu ya polisi, aliwaagiza wataalamu wa kimtandao wadukue tukio hilo na wafahamu wapi muuaji alipo muda huo.

Walifanikiwa, lakini ni mbali mno. Haraka jeshi la askari polisi na wataalamu wachache wakatoka, Inspekta Kasese pia akapewa taarifa mpya kuwa ni pahala gani anapopaswa kuelekea, safari ikabadilika, sasa walimfuatilia muuaji halisi aliyeamua kujitokeza hadharani mwenyewe, tena akiwa na mtu waliyemshuku wao kwa asilimia zote. Jakota, ndipo alama ziliwaonesha muuaji yupo huko. Ni porini mno, tena ilikuwa nje kidogo ya jiji lao la SENI, Walipafuata. Swali, muuaji ana kusudio gani kujionesha leo hii? Kwanini pia awe na Labi Kimati aliye katika hali mbaya! Hali iliyoiegesha shingo yake karibu kabisa na panga la malaika mtoa roho! Baada ya salamu ile, mzee huyo muuaji akaanza kuongea. "Hata Mimi moyo wangu unaniuma kumtendea haya kijana ambaye sasa amebadilika, sio yule mnyama aliyenifanya niishi hivi leo hii." aliweka tuo, macho pima akiitazama kamera.

**Tukutane toleo lijalo.**



# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (05)- Na: Eva Mrema

***Ilipoishia….***

**Mimi Sunche nakupenda sana bibie" sauti ilitamatika na kiwiliwili cha mwenye nayo kikaanza kujitokeza taratibu jukwaani. "Nikiambiwa niandike shairi juu ya uzuri wako, pengine halitapimika kwa mizani mizuri ya kiandishi, lakini nataka kuweka kumbukumbu hii moyoni mwako….**

---

***Endelea...***

Kwenye sifa kumi za mwanamke niliyemuota, umeongeza mpya ambayo sikuwahi kuiota.

Wewe ni mzuri wa sura na umbo kama kiota. Wewe ni mng'aavu wa moyo na macho kama nyota. Huo urefu, wa twiga kwenye mbuga nzuri ya ngorongoro 'ndo urefu wa mahusiano yetu, yaso robo ya migogoro, nakutaka kwenye moyo wangu, uingie na lako godoro, njia kuu itakuwa chaguo la kudumu, pasi na moja chochoro,



Dunia ina kila kitu kwa ajili ya kila mtu,
Wewe ni kila kitu kwa ajili ya mimi tu!
Usijishushe thamani wala kujipunja wako utu,
Ukubwa wa penzi lako kwangu nimekuwa kisu butu,
Nakupenda Tabita, Utakacho nitatafuta,
Uendako nitakufuata, Basi usinifanyie utata,
Maana kwa hakika, mimi ninakutaka!"

Kila mtu aliyesikiliza maneno ya Sunche kama hakumjua kabla angesema ni mbongo, tena kutokea Tanga Tanzania kule inakosemekana mapenzi ndiko yalikozaliwa. Makofi na nduru vilithibitisha utamu wa maneno niliyosikilizishwa kwa kughaniwa mithili ya utenzi, Tabita mie' katikati ya masikio mengi yaliyosikia pia.

Filamu yangu bora kabisa ya mahaba ilibadilika na kuwa maisha yangu ndani ya hizi dakika za kufunuliwa moyo na Sunche. Nilinyanyua hatua, naye alijongea, tulikutana katikati kama mkanda. Alinikumbatia kwa kumaanisha nami nililipa fadhila. Chozi japesi lilinitoka. Nilitamani kulalamika ila nikajizuia tu na kuiacha furaha itamalaki. "Nakupenda sana" aliniambia tena. Nilimjibu kuwa nampenda sana" picha zilipigwa na kumbukumbu juu ya furaha ile zilihifadhiwa. Nilianza kupiga hatua ili nikaketi, Sunche aliukamata mkono wangu na kuniomba nisubiri. "Vya kunishangaza havijaisha tu?" Niliuliza hali nikitabasamu. Alizamisha mkono kwenye mfuko wa koti kubwa alilokuwa amevaa na kutoa kikasha cha zawadi chenye ukubwa wa sentimita kumi na tatu. Kilifungwa na mfungaji nguli wa zawadi. Alinipatia nifungue mwenyewe. Mapigo ya moyo yaliongeza kasi. Nywele zilinisimamа, sikuelewa hata ni kwanini. Nilimtazama Sunche ambaye hakuonesha hisia yoyote ya wazi juu ya kikasha kile…

Moyo ulinidunda kwa shauku, papi za midomo yangu ziliminyana huku mashavu yakinyooka kuelekea nyuma kwa tabasamu. Nilianza kufungua kikasha kile cha zawadi. Niliutoa uzi mpana wa plastiki kwa mbwembwe zote. Kisha nikalifunua karatasi la kumeremeta na kuliacha mkononi chini ya kikasha kile. Nikaanza sasa kukifungua kikasha. Kikasha kilitii na kufunguka vizuri kabisa. "*Ooh! My God*" nilirukaruka na kumkumbatia Sunche. Moja ya ndoto ya mwanamke yeyote mwenye umri wa kufanana na wangu ni kupata mtoto. Aisee zawadi niliyopewa ilinipenya mpaka kumoyo. Mimi ni mtu naamini sana kwenye ishara, kunipa mimi zawadi ya kiatu cha mtoto ilimaanisha


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (05) - Na: Eva Mrema

ni mtu mwenye ndoto nyingi na mimi. "Vuta kamba ndani ya kiatu" Sunche aliniambia. Nami si' nikaivuta bwana! Weeeehhhh! "Nini hiki jamani! Nilishindwa kustahimili. Machozi membamba yalianza kunitoka japo yalisalia machoni. Tabasamu halikunitoweka, liliufanya uso wangu umchanganye kila aliyenitazama. Sunche alikamata kamba ile ndogo ya kiatu cha mtoto na kuanza kuifungua taratibu ili iachilie kitu. Macho hayakunitoka peke yangu, kila aliyekuwepo eneo lile machoye yalimtoka pima. Binafsi viganja vya mikono yangu viliyashikilia mashavu yangu kwa shauku, ungesema nayazuia yasidondoke. Tayari niliona kilichoshikwa ila kuna muda nilihisi ni ndoto tu

"Pete!" Jamani ni pete! Habari zilitembea na kila aliyezisikia alishangilia na kujongea karibu. Sunche aliishika vizuri pete ile. Alipiga goti moja chini na mguu mmoja aliunyoosha na kuutumia kama egemeo la kiwiko cha mkono wake wa kushoto. Aliishika pete na mkono wa kulia na kunitazama kwa upendo wa hali ya juu. "Tabita, naomba uwe mchumba wangu, rasmi" kauli iliyofumbua kinywa chake ilinisisimua sana.
Nilizunguruka kama Sinderela aliyekusudia kuonesha upana wa gauni lake. Niligeuka na kusema "ndio" kwa kinywa changu.

Nilikuwa na miaka thelathini na miwili, na hii ilikuwa mara yangu ya kwanza kuchumbiwa, hisia zote mvurugiko zilitoweka. Nilihisi jambo moja tu kwa uhakika; Tabita nimependwa. Sherehe ya watu tukaizima kwa matukio yetu ya kushtukiza. Pete ilipenya kidoleni na kukaa kitako. Ni kama muundaji alitumia kidole changu kama kipimio wakati akiiunda. Ilikuwa nzuri sana. Pete ya dhahabu halisi iliyong'azwa na kito cha almasi na nakshi za tanzanite. Niliutazama mkono wangu na kumuonesha kama vile namringishia. Sunche aliukamata na kuubusu kwa mahaba huku akiusugua sugua. Alinyanyuka pale chini na kunibusu kwenye paji la uso wangu. Nilimkumbatia na moyoni yalizalika maneno niliyojizuia kutamka. Asante kwa kunichumbia? Ulikuwa wapi Sunche wakati manyang'au yakiniparura? Nakupenda kuliko nafsi yangu? Hapana kwa kweli maneno haya yataua *'brand'* ya familia kabisa. Nilijikaza na kubaki na maneno yangu matamu yaliyobeba shauku za kizamani. Sherehe ilibamba vizuri mno.

*Tuliruka kwanja* kwa mioyo mikunjufu kabisa. Baada ya muda, tafrija ilifika ukomo, ndo kwanza saa nne usiku; nilitamani mno kuimba na kucheza. Kwa nilivyokuwa nimefurahi ningezaliwa na kukulia katika jiji lile kubwa uwezekano wa kuwa msanii wa muziki ulikuwa ni mkubwa sana. Asante wazazi wangu walioniambia kila mara mziki ni uhuni. Nilitoa maoni juu ya wapi twende japo hayakupokelewa na Sunche aliyekuwa akiendesha gari.


Dakika arobaini na tisa, zilitutosha kuingia nyumbani kwa Sunche wangu. Niliridhia kila lililotoka kwake maana nina uhakika ananipenda. Taa zilizimwa nje wala ndani hakukuwa na nuru. Nikaanza kujijaza mawazo, labda tanesco wamefanya yao. Labda Sunche alisahau kuwasha taa. Aahh! Niliamua nitulie kama mbwa mgeni, baada ya kuona siwezi kubadilisha kitu. Nilifunguliwa mlango na kushuka garini. Nilingoja amalize kuchukua vitu alivyokuwa akichukua garini. Alishangaa hali ya kutokuwa na umeme. Uliwaka nyumba zote za jirani kasoro kwake tu. Alipiga mluzi na kisha kufungua mlango mkubwa wa sebuleni. Kila kitu kiliwaka kwa ghafla.
Namaanisha kila kitu kiliwaka …..

**SURA YA NNE.**

Taa zote za nyumba ziliwaka sambamba na taa za moyo wangu. Macho yalichekelea kwa kile yalichokiona. Akili ilinikumbusha kuwa nimefanya uamuzi sahihi kuchukua hatua ya kwanza, kuelekea mishangao hii ninayokutana nayo ya kufurahisha. Maandalizi haya sijui yalifanywa saa ngapi. Nyumba ilipambwa kuliko ukumbi wa harusi. Maua mekundu yalitapakaa chini tulipopakanyaga mdogomdogo kama tunapaogopa. Meza yenye ukubwa wa upande mmoja wa kanga ilikuwa mbele ya macho yetu. Ilipambwa vizuri na mpambaji stadi. Iliwekwa vinywaji vya kuvutia sana, kiufupi kuelezea kila nilichokiona ni kupunguza utamu wa ule muonekano.

*Itaendelea...*

# Tangazo




www.richardmwambe.com

JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com